**COVID-19 Taarifa Muhimu**

**Department of Social and Health Services** inasaidia kuzuia na kudhibiti COVID-19. Tunajali sana afya na usalama wa wateja wetu. Tunafuata agizo la Gavana Inslee la *Kaa Nyumbani, Kuwa na Afya* na mpango wa urejesho.

Tuna huduma za lugha bila malipo. Huduma hizi ni pamoja na wakalimani na tafsiri, na habari iliyoandikwa katika miundo mingine. Ikiwa unahitaji msaada kupata huduma zetu, tafadhali piga simu kwa DSHS **800-737-0617** na uchague chaguo la 4. Unaweza pia kupiga simu kwa **711** kwa Huduma ya Uwasilishaji wa Washington.

COVID-19 imeathiri vipi mipango na huduma za DSHS?

## Msaada wa Uzee na wa Muda Mrefu

COVID-19 inaweza kuwa hatari sana kwa wakazi wa vituo vya utunzaji wa muda mrefu. Mnamo tarehe 12 Mei, nyumba za kuwatunza wazee, vituo vya kuishi na nyumba za familia za watu wazima haziruhusu wageni. Hizi sheria zinaweza kubadilika wakati wa janga.

Unaweza kuona sheria za wageni kwa vifaa vya utunzaji kwa kutembelea ukurasa wa tovuti wa FamHelp. Ukurasa huu wa tovuti pia unaorodhesha vituo vya utunzaji na kesi za COVID-19 zilizoripotiwa. Ikiwa una maswali kuhusu vituo vya utunzaji wa muda mrefu, tafadhali piga simu kwa 888-856-5691. Saa zetu ni kati ya saa 12 asubuhi (6 a.m.) na saa 4 usiku (10 p.m.)

Ofisi ya Viziwi na wenye Ugumu wa Kusikia huwahudumia wateja ambao ni viziwi, viziwi-vipofu au wenye ugumu wa kusikia. Wao pia hufanya kazi na watoa huduma. Ikiwa una mteja mwenye uziwi anayehitaji msaada wa mawasiliano, tafadhali wasiliana na ofisi.

- Barua pepe: ODHHCOVID-19@dshs.wa.gov
- Simu: 360-338-6042
- Kwa TTY/TDD: 360-725-3455
- Ikiwa wapiga simu hawana ufikiaji wa TTY/TDD, tafadhali piga simu kwa 711
- Tovuti ya ODHH

## Behavioral Health Administration

Behavioral Health Administration huwahudumia watu wazima na watoto katika hospitali tatu za akili za jimbo, Special Commitment Center na Office of Forensic Mental Health Services.

Tumesitisha ziara katika maeneo haya ili kuzuia kuenea kwa COVID-19. Tunazo huduma za umbali za video kwa wateja wakati inapofaa. Kuuliza kuhusu sera ya mgeni au kwa maswali mengine, tafadhali piga simu:

- Western State Hospital – **253-582-8900**
- Eastern State Hospital – **509-565-4000**
- Child Study and Treatment Center – **800-283-8639**

- Office of Forensic Mental Health Services
  - Maple Lane – **360-664-4641**
  - Yakima – **253-582-8900**
  - Fort Steilacoom – **253-984-5651**
- Special Commitment Center– **253-588-5281, mkondo 0095**

**<u>Division of Vocational Rehabilitation</u>**
Tumefunga ofisi za Division of Vocational Rehabilitation kwa sasa.

- Washauri watatoa huduma na msaada kupitia simu.
- Nambari ya simu ya sasisho za huduma: **800-637-5627**

**<u>Developmental Disabilities Administration</u>**
Kumbi za ofisi zimefungwa kwa sasa. Fircrest School, Lakeland Village, Rainier School na Yakima Valley School haziruhusu wageni kwa wakati huu. Tafadhali piga simu ukitumia nambari zilizoko hapa chini ikiwa una maswali.

- Tunaweza kutoa huduma kwa umbali na idhini ya awali kutoka kwa msimamizi wa kesi ya DDA.
- Tathmini zinaweza kufanywa kwa umbali na ratiba ya kukamilisha tathmini inaweza kuongezwa muda kwa msingi wa kesi moja baada ya nyingine.
- Kwa huduma katika Island, King, San Juan, Skagit, Snohomish na Whatcom, piga simu: 800-314-3296.
- Kwa huduma katika Clallam, Clark, Cowlitz, Grays Harbor, Jefferson, Kitsap, Lewis, Mason, Pacific, Pierce, Skamania, Hudston au Wahkiakum, piga simu: 800-248-0949
- Kwa huduma katika kaunti zingine zote za jimbo, piga simu 800-462-0624

**<u>Economic Services Administration</u>**

<u>CHILD SUPPORT:</u> Kumbi za Division of Child Support zimefungwa kwa sasa. Ili kupata habari ya kesi au fanya malipo, piga simu **800-442-KIDS (5437).** Waajiri ambao wanahitaji kuripoti kufuta kazi au kufungwa wanaweza kupiga simu kwa **800-562-0479**.

<u>OFISI ZA HUDUMA ZA JUMUIYA:</u> Huduma chache zinapatikana **kwa miadi pekee. Unaweza**:

- Kuchukua kadi ya EBT ikiwa una huduma za barua za uwasilishaji wa jumla au wewe ni mpokeaji wa chakula kilichoharakishwa.
- Kuchukua huduma za msaada wa dharura.
- Kuwacha makaratasi.

<u>KITUO CHA MAWASILIANO CHA HUDUMA YA WATEJA:</u> Pata huduma kwa kupiga simu **877-501-2233**. Unaweza:

- Tuma ombi la faida.
- Pata taarifa ya kesi au mabadiliko ya ripoti.
- Kamilisha uhakiki wa ustahiki au uthibitisho wa kati.

- Omba kadi mpya ya EBT.
- Fikia kesi ya WorkFirst au mfanyakazi wa kijamii.

WASHINGTON CONNECTION: Watu wanaweza kupata huduma za mtandaoni kwa Kiingereza na Kihispania. Nenda kwa WashingtonConnection.org kuomba faida, hakiki kamili, ripoti za mabadiliko na upate huduma zingine za karibu.

MIPANGO YA UELEKEZAJI YA WAZEE, VIPOFU AU WALEMAVU/MAKAZI NA MAHITAJI MUHIMU: Tumeahirisha ukaguzi wa ulemavu wa ABD kwa sasa. Tumebadilisha pia sheria za uelekezaji wa HEN na kusimamisha baadhi ya ufuatiliaji unaohitajika. Tafadhali piga simu **877-501-2233** kwa taarifa zaidi kuhusu kesi za HEN na ABD.

CHAKULA CHA MSINGI: DSHS imeongeza faida za chakula kwa kiasi kikubwa kinachoruhusiwa kwa saizi ya kaya kwa mwezi wa Machi hadi Mei 2020. DSHS itaomba serikali ya shirikisho nyongeza ya chakula cha dharura kila mwezi wa COVID-19.

- *Ajira na Mafunzo ya Chakula cha Msingi:* Mipango na huduma zote za BFET zinapatikana. Washirika wa BFET hutoa huduma kupitia simu na mtandaoni.
- *Watu Wazima Wanaojiweza bila Wategemezi:* Mahitaji ya kazi ya ABAWD hayahitajiki kwa sasa. DSHS bado inaelekeza watu ambao wako tayari na wana uwezo wa kushiriki.

UHAKIKI WA FAIDA: DSHS iliongeza ukaguzi wa ustahiki ambao ulitarajiwa Aprili, Mei au Juni 2020 kwa miezi sita. Uhakiki wa uthibitisho wa kati uliotarajiwa Aprili, Mei au Juni 2020 haufai kukamilika. Faida zitaendelea mradi kaya yako itakidhi mahitaji mengine yote ya kustahiki.

DISASTER CASH ASSISTANCE PROGRAM: DCAP inapatikana kwa familia na watu wasio na watoto. Sio lazima uwe raia. Watu wanastahiki ikiwa wanakidhi vikomo vya mapato na rasilimali, na hawastahiki mipango mingine ya pesa. Piga simu **877-501-2233** kupata maelezo zaidi.

OFFICE OF REFUGEE AND IMMIGRANT ASSISTANCE: ORIA ina mipango ya kusaidia wakimbizi na wahamiaji:

- Kutafuta kazi na mafunzo.
- Msaada wa uhamiaji.
- Ushauri wa vijana.
- Msaada kwa wakimbizi wazee, watoto, wanafunzi, na wengine.
- Mipango ya kawaida hufunguliwa kwa umbali wakati wa COVID-19. Ofisi ina huduma mpya za kukusaidia kuomba kazi au ukosefu wa ajira, kusaidia elimu yako, na kutoa msaada wa makazi. Usaidizi wa Fedha kwa Wakimbizi na ustahiki wa Msaada wa Matibabu kwa Wakimbizi umeongezwa muda hadi tarehe 30 Septemba 2020.
- Kwa huduma na habari zaidi, piga simu **360-890-0691**.

TEMPORARY ASSISTANCE FOR NEEDY FAMILIES/WORKFIRST: TANF Upanuzi wa Muda wa miezi 60 sasa unajumuisha ugumu kwa sababu ya COVID-19.

- Mahitaji ya WorkFirst yamesitishwa kwa sasa. Wateja wanaweza kuendelea kushiriki ikiwa wana uwezo.
- Tumesitisha vikwazo vya WorkFirst kwa sasa. Tumesitisha pia ziara za nyumbani na wafanyakazi.
- Ikiwa wewe ni mshiriki wa Kazi za Jumuiya au wa masomo kazi ya WorkFirst, utabaki kuajiriwa na kulipwa hata kama huwezi kushiriki kutokana na COVID-19.